

UMUHIMU WA KUZINGATIA TARATIBU ZA RUFEE KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Imetolewa na ofisi ya Rais, Tume ya utumishi wa Umma

1.0. Ni wajibu wa nani kuzingatia taratibu za rufaa

Mrufani na Mrufaniwa wote wanawajibu wa kuhakikisha kuwa wanazingatia Taratibu za rufaa katika Utumishi wa Umma. Ili mchakato mzima wa rufaa uweze kukamilika pande zote mbili, yaani mrufani na mrufaniwa wanalo jukumu la msingi na la kisheria kuhakikisha kuwa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazohusu rufaa zinazingatiwa ipasavyo. Bila kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za rufaa haki na usawa katika utumishi wa umma haiwezi kupatikana, hivyo suala la uzingatiaji wa sheria ni suala la msingi sana. Lengo Kubwa la kuzingatia taratibu hizi ni kuimarisha na kuboresha utawala bora katika uendeshaji wa shughuli za serikali.

2.0. Ni zipi taratibu za rufaa katika utumishi wa umma.

2.1. Utaratibu wa Rufaa za watumishi wa Umma umeanishwa kwenye Kifungu cha 25(1) (a) – (e) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebisha na sheria Na. 18, 2007 kikisomwa pamoja na Kanuni Na.60(1) – (5) cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 kama ifuatavyo:-

2.1.1. Kanuni ya 60(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 inawataja watumishi walioteuliwa na Rais ambao Mamlaka zao za nidhamu ni Katibu Mkuu

Kiongozi kuwa watakata rufaa kwa Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

2.1.2. Kanuni ya 60(2), (3) na (5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 inawataja watumishi wengine wote isipokuwa walio katika masharti ya huduma ya kawaida watakata rufaa kwa mara ya kwanza kwenye Tume na kama hawataridhika na uamuzi wa Tume watakata rufaa kwa Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

2.1.3. Kanuni ya 60(4) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 inawataka watumishi wa masharti ya huduma za kawaida kukata rufaa kwa kuzingatia Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na.6 ya mwaka 2004.

3.0. Mchakato wa rufaa

- 3.1. Kwa mujibu wa Kanuni 61(1) mtumishi wa Umma ambaye hajaridhika na uamuzi wa Mamlaka ya Nidhamu anapaswa kukata rufaa katika kupindi cha siku 45 tangu tarehe ya kukabidhiwa uamuzi wa Mamlaka ya Nidhamu na nakala ya rufaa ipelekwe kwa Mamlaka ya Nidhamu inayokatiwa rufaa.
- 3.2. Kanuni 61 (2) inaelekeza wajibu wa Mamlaka ya Rufaa kupeleka nakala ya rufaa kwa Mamlaka ya Nidhamu inayokatiwa rufaa isipokuwa pale tu ambapo imejiridhisha kuwa nakala hiyo ipo pia kwa Mamlaka ya Nidhamu husika.
- 3.3. Kanuni 61(3) inaelekeza kuwa baada ya kupokea nakala ya rufaa kutoka kwa mrufani au Mamlaka ya rufaa, Mamlaka ya Nidhamu inapaswa kuwasilisha mwenendo na vielelezo vya shauri kwa Mamlaka ya Rufaa katika muda wa siku 14 tangu

tarehe ya kupokea nakala ya rufaa. Nakala ya mwenendo na vielelezo atapewa mrufani.

- 3.4. Kanuni 61(4) inaelekeza kuwa Mamlaka ya Rufaa inaweza kupokea rufaa iliyoletwa nje ya muda iwapo kutakuwa na maelezo/sababu za kuridhisha kuhusu chanzo cha kuchelewa.
- 3.5. Kanuni 62(1) inaelekeza kuwa Mrufani na Mrufaniwa wanaruhusiwa kusikilizwa ama kwa maandishi au kwa kuhudhuria na kujieleza.
- 3.6. Kanuni 62(2) inatoa fursa kwa mamlaka ya rufaa kuamua rufaa yoyote pasipo kuwapo na Mrufani. Aidha, rufaa lazima iamuliwe ndani ya siku tisini (90) kuanzia tarehe ya kupokelewa kwa vielelezo muhimu vya rufaa.
- 3.7. Kanuni 63 inaelekeza kuwa katika kila rufaa ambayo uamuzi anapewa mrufani, Mrufaniwa (Mamlaka ya Nidhamu) ana haki ya kupewa nakala ya uamuzi.
- 3.8. Kanuni ya 64(1) inaelekeza kuwa uamuzi wa Rufaa lazima utekelezwe, na anayekataa kufanya hivyo atastahili kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

4.0. **Changamoto**

Zipo changamoto kadhaa ambazo Tume inakabiliana nazo katika suala la uzingatiaji wa taratibu za rufaa kama ifuatavyo:-

- 4.1. Suala la elimu kwa wadau, pamoja na jitihada ambazo Tume imekuwa ikizifanya kutoa elimu kwa wadau wake, bado kuna umuhimu na ulazima wa kutoa kipaumbele katika eneo hili ili kuongeza ufahamu wa taratibu za Rufaa katika Utumishi wa Umma.
- 4.2. Mamlaka za Nidhamu kutozingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali kuhusu uzingatiaji wa Taratibu za rufaa.

4.3. Ucheleweshwaji wa vielelezo na nyaraka za mashauri ya nidhamu kutoka katika Mamlaka za Nidhamu. Hili ni tatizo la muda mrefu ambalo Tume inakabiliwa nalo ili kuhakikisha kuwa rufaa zinasikilizwa ndani ya muda wa siku tisini (90), muda uliowekwa kisheria.

Mamlaka za nidhamu zinapaswa kutoa ushirikiano katika kushughulikia rufaa na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu katika uendeshaji wa mashauri ya nidhamu na rufaa.

Kwa maoni, maswali au ushauri tafadhali tuandikie :

Katibu

Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

S.L.P 9143

Dar Es Salaam